## MUHTASARI WA KIKAO CHA BODI YA ZABUNI KILICHOFANYIKA TAREHE 22/11/2021 KWENYE UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI

**A. WALIOHUDHURIA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndugu Clovis Mrutu | -Afisa Uchaguzi (W) | -Mwenyekiti |
| 2. | Ndugu Peter Luhanda | -Afisa Ugavi (W) | -Katibu |
| 3. | Ndugu Dafrosa Mkenda | -A/Elimu Sekondari (W) | -Mjumbe |
| 4. | Ndugu Alex Mang'ara | -Afisa Mipango (W) | -Mjumbe |
| 5. | Shaban O. Gwandu | -Afisa Elimu Msingi (W) | -Mjumbe |

**B. WAALIKWA:**

| | | | |
|---|---|---|---|
| 1. | Ndugu Innocent Nsojo | -Afisa Ugavi | -Sekretariati |
| 2. | Ndugu Frank Herman | -Mhandisi Ujenzi | -Mwalikwa |

**BZ/KIL/1/11/2021: KUFUNGUA KIKAO**

Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe kwenye kikao. Aliwaomba ushirikiano wajumbe wote, alisisitiza uwazi wakati wa kujadili hoja, kikao kilifunguliwa rasmi mnamo saa 7:00 Mchana.

**BZ/KIL/2/11/2021: KUTHIBITISHA AGENDA**

Mwenyekiti alimtaka Katibu kusoma agenda za kikao ili wajumbe wazipitie, baada ya wajumbe kuzipitia agenda hizo waliridhia kuwa ndizo ziwe agenda za kikao cha tarehe 22/11/2021

1. Kufungua kikao
2. Kuthibitisha agenda
3. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha tarehe 13/09/2021
4. Ombi la idhini ya Ujenzi na ununuzi wa vifaa katika mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO -19 Idara ya Elimu Msingi kwa kutumia njia ya manunuzi ya *Force Account*
5. Ombi la idhini ya Ujenzi na ununuzi wa vifaa katika mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya UVIKO -19

| ............ | 08/12/2021 | ............ |
|---|---|---|
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

Idara ya Elimu Sekondari kwa kutumia njia ya manunuzi ya *Force Account*

6. Ombi la kupitisha wazabuni wa kutoa huduma ya kuuza Mbao katika miradi Ujenzi wilaya ya Kilindi

7. Mengineyo

8. Kufunga kikao

**BZ/KIL/3/11/2021: KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA TAREHE 13/09/2021**

Katibu alisoma muhtasari wa kikao cha tarehe 13/09/2021 ili wajumbe wajiridhishe na Muhtasari huo na pia kwa madhumuni ya kufanya marekebisho Kabla haujasainiwa, Baada ya Katibu kusoma Muhtasari huo wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo ni sahihi kwa ajili ya kumbukumbu za Ofisi.

**BZ/KIL/4/11/2021: OMBI LA IDHINI YA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KATIKA MRADI WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19 IDARA YA ELIMU MSINGI KWA KUTUMIA NJIA YA MANUNUZI YA *FORCE ACCOUNT***

Katibu aliwasilisha taarifa katika kikao kuwa amepokea ombi la idhini ya kujenga na kununua vifaa vya ujenzi kwa kutumia njia ya manunuzi ya '*Force Account*' kutoka katika Idara ya Elimu Msingi kupitia fedha za mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19.

Maelezo yalitolewa kuwa, Idara ya Elimu Msingi imepokea kiasi cha Tshs. 2,700,000,000.00 ikiwa nifedha ya Ujenzi wa Madarasa 131 pamoja na Ujenzi wa Bweni moja. Hivyo Idara inaomba kutekeleza miradi hiyo kwa kutumia njia ya Force Account.

Halmashauri katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 imepokea fedha za Mradi kutoka Serikali kuu, hivyo Halmashauri imejipanga

| | | |
|---|---|---|
| ...........[signature]........... | 08/12/2021 | ...........[signature]........... |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |

kutekeleza ujenzi kupitia fedha hizi za mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19 kama ilivyoelekezwa.

Idara ya Elimu Msingi inaomba Bodi ya Zabuni kutoa Idhini ya kupitisha njia ya Manunuzi ya Force Account katika miradi hii ya Maendeleo.

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa na kuijadili. Bodi ya Zabuni imepitisha maombi ya Idara ya Elimu Msingi. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/5/11/2021: OMBI LA IDHINI YA UJENZI NA UNUNUZI WA VIFAA KATIKA MRADI WA MAENDELEO YA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UVIKO - 19 IDARA YA ELIMU SEKONDARI KWA KUTUMIA NJIA YA MANUNUZI YA *FORCE ACCOUNT***

Katibu aliwasilisha taarifa katika kikao kuwa amepokea ombi la idhini ya kujenga na kununua vifaa vya ujenzi kwa kutumia njia ya manunuzi ya '*Force Account*' kutoka katika Idara ya Elimu Sekondari kupitia fedha za mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19.

Maelezo yalitolewa kuwa, Idara ya Elimu Sekondari imepokea kiasi cha Tshs. 1,300,000,000.00 ikiwa nifedha ya Ujenzi wa Madarasa 65 katika Shule za Sekondari. Hivyo Idara inaomba kutekeleza miradi hiyo kwa kutumia njia ya Force Account.

Halmashauri katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 imepokea fedha za Mradi kutoka Serikali kuu, hivyo Halmashauri imejipanga kutekeleza ujenzi kupitia fedha hizi za mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19 kama ilivyoelekezwa.

Idara ya Elimu Sekondari inaomba Bodi ya Zabuni kutoa Idhini ya kupitisha njia ya Manunuzi ya Force Account katika miradi ya Maendeleo.

| | | |
|---|---|---|
| ......................... | 08/12/2021 | ......................... |
| **Mwenyekiti** | **Tarehe** | **Katibu** |

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa na kuijadili. Bodi ya Zabuni imepitisha maombi ya Idara ya Elimu Sekondari. Ombi limekubaliwa.

**BZ/KIL/6/11/2021: OMBI LA KUPITISHA WAZABUNI WA KUTOA HUDUMA YA KUUZA MBAO KATIKA MIRADI UJENZI WILAYA YA KILINDI**

Katibu aliwasilisha taarifa katika kikao kuwa kitengo cha Manunuzi na Ugavi kinaomba Idhaini ya kupitishwa kwa Wazabuni wa kutoa huduma ya kuuza na kusambaza Mbao katika wilaya ya Kilindi.

Maelezo yalitolewa kuwa, Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kimewasilisha Orodha hii kufuatia Halmashauri yetu kupokea Fedha nyingi kwa ajili ya Miradi ya Ujenzi wa Madarasa na Miundombinumingine ya Elim una Afya katika kipindi kifupi, na hivyo miradiyote hiyo inatakiwa kutekelezwa kwa wakati mmoja hivyo kufanya mahitaji ya Mbao kuwa makubwa sana kiasi cha kuhitaji wazabuni ambao wataweza kutoa huduma hiyo kwa ufanisi.

Halmashauri katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka 2021/2022 imepokea fedha za Mradi kutoka Serikali kuu, hivyo Halmashauri imejipanga kutekeleza ujenzi kupitia fedha hizi za mradi wa Maendeleo ya Ustawi wa Taifa na mapambano dhidi ya UVIKO -19 na fedha nyingine za Miradi ya Maendeleo katika bajeti ya mwaka huu kama ilivyoelekezwa.

Kitengo cha Manunuzi na Ugavi kinawasilisha Majina yafuatayo ambayo Kitengo kitawatumia katika mchakato wa kupata wazabuni wa kutoa huduma ya Mbao Wilayani, majina hayo ni kama Ifuatavyo; - M/s John Raphael Machocho wa Songe -Kilindi, M/s John B. Shayo wa Handeni, M/s Gaitani M. Mlumbe wa Mafinga-Iringa, M/s Stanile Mangulla wa Mafinga-Iringa, M/s Nesto N. Sanga wa Mafinga-Iringa, M/s Madiga Group (T) Limited wa Dar Es Salaam, na M/s Nassa Upendo Mart Trader wa Tanga.

Wajumbe wa Bodi ya Zabuni walipokea taarifa na Kuipitisha wazabuni wote. Ombi limekubaliwa.

| | | |
|---|---|---|
| ............................ | 08/12/2021 | ............................ |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |

BZ/KIL/7/11/2021: MENGINEYO

Kabla ya kufunga kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kujadili mambo mengineyo ambayo yataboresha utendaji wa kazi za Bodi ya zabuni, wajumbe walishauri kuwa katika utekelezaji wa Miradihii Halmashauri izingatie Miongozo iliyotolewa ya Maelekezo ya Matumizi ya Fedha hizi ili kuweza kutekeleza kwa Ufanisi na kupata thamani ya fedha katika miradiiliyo bora.

BZ/KIL/8/11/2021: KUFUNGA KIKAO.

Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kutoa michango yao ya mawazo yenye tija kwa ustawi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi, na kikao kilifungwa rasmi mnamo saa 08.00 Mchana.

| | | |
|---|---|---|
| .............................. | 08/12/2021 | .............................. |
| Mwenyekiti | Tarehe | Katibu |



CamScanner